## BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

National Council for Technical and Vocational Education and Training

## TAARIFA KWA UMMA

## UDAHILI WA WANAFUNZI KATIKA MKUPUO WA MACHI 2026/2027

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linapenda kuufahamisha umma kuwa udahili wa wanafunzi katika ngazi ya Astashahada na Stashahada kwa kozi zote, **isipokuwa kozi za Afya** Tanzania Bara, umeanza **tarehe 10 Februari, 2026 na utakamilika tarehe 28 Februari 2026**. Udahili huu unahusu vyuo vilivyosajiliwa, kuthibitishwa na kuidhinishwa na Baraza kuwa na uwezo wa kupokea wanafunzi.

Wahitimu wote wa Elimu ya Sekondari pamoja na wahitimu wa vyuo wenye sifa za kujiunga na kozi za Astashahada na Stashahada wanashauriwa kuwasilisha maombi yao moja kwa moja katika vyuo wanavyovipenda. Waombaji watakaochaguliwa watawasilishwa NACTVET kwa ajili ya uhakiki.

Baraza linaelekeza vyuo kuhakikisha vinazingatia sheria, kanuni na taratibu za udahili, pamoja na kuifuata Kalenda ya Udahili inayopatikana katika tovuti ya Baraza.

Aidha, Baraza linawakumbusha waombaji kuhakikisha wanaomba kujiunga na vyuo vilivyosajiliwa na kuidhinishwa na Baraza kudahili wanafunzi katika muhula wa Machi, 2026.

Orodha ya vyuo vilivyoruhusiwa kufanya udahili inapatikana katika tovuti ya NACTVET ambayo ni **www.nactvet.go.tz.**

**IMETOLEWA NA OFISI YA KATIBU MTENDAJI**
**NACTVET**
**13/02/2026**